



HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO

SHULE YA SEKONDARI PRINCE CLAUS
S. L. P. 82,
Lushoto.
02/01/2021

Kumb Na. PC**SS/FS/V.1/2021/001**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI
PRINCE CLAUS MWAKA 2021**

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga Kidato cha kwanza kwa mwaka 2021 katika Shule ya Sekondari Prince Claus iliyopo Kata ya Magamba Tarafa ya Lushoto, wilaya ya Lushoto mkoa wa Tanga.

Soma maagizo kikamilifu yenye kurasa tatu ili uyakamilishe kabla ya kujiunga na shule kwa tarehe iliyotajwa (shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 na wewe utafika shuleni tarehe hiyo kulingana na maagizo, utafika shuleni tarehe 11/01/2021 saa 1.00 asubuhi.

Prince Claus Shule ya Sekondari ni shule ya kutwa, hivyo utakaa nyumbani na wazazi wako au ndugu zako lakini utalazimika kufuata Sheria, Taratibu na Miongozo ya shule kama utakavyoelekezwa na walimu utakapofika rasmi shuleni.

Fika na Fomu iliyojazwa na Mganga wa Hospitali (**imeambatanishwa**). Vilevile fika na fomu iliyoambatanishwa kwa ajili ya Mzazi kuijaza kukubali Sheria, Kanuni na Taratibu za Shule.

Asante

□□□□□□□□□□

Yona Ndekirwa

Mkuu wa Shule

Ukurasa 1

Mahitaji ya Shule

A. Sare ya Shule:

1. Mashati 2 meupe ya mikono mifupi, Tetroni (lisiwe linalobana au kuona ndani), **masweta 2 ya rangi damu ya Mzee**
2. Mvulana ashone Suruali 2 ndefu za **Heshima** (***Vimodo Haviruhusiwi***) za Kitambaa cha rangi nyeusi, soksi nyeusi na Msichana ashone Sketi 2 Ndefu za Kitambaa cha rangi ya karoti, soksi nyeupe
3. Kila mwanafunzi anunue viatu vya **Ngozi vyeusi Pea 2** ambavyo **hupakwa kiwi na Kufungwa kamba**. Visiwe vyenye visigino virefu au buti.

B. Vifaa vya Shule:

Zana za Kazi

- a). Dictionary
- b). Mkebe wa Hisabati
- c). Daftari 11za masomo na 11 za mazoezi kubwa na kalamu

Mkuu wa Shule.
Prince Claus

Ukurasa 2

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



Ofisi ya Raisi □ Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Prince Claus Shule ya Sekondari, S. L. P. 82 Lushoto.

